# Dhima za Mbolezi za Sasa katika Jamii ya Wakinga Waishio Makete, Tanzania

Tumaini Juma Sanga
Chuo Kikuu cha St. John cha Tanzania

**Ikisiri**

Mbolezi ni kipengele muhimu katika utamaduni wa mazishi miongoni mwa jamii za Afrika. Makala hii inalenga kujadili dhima za mbolezi katika jamii ya Wakinga waishio wilaya ya Makete, mkoani Njombe. Uchambuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kibantu. Makala hii inadhihirisha kuwa tafiti zilizotangulia zilieleza kuwa dhima kuu ya mbolezi ni kuliwaza. Makala hii imebaini kuwa mbolezi katika jamii ya Wakinga zina dhima mbalimbali. Baadhi ya dhima hizo ni kuliwaza wafiwa, kuendeleza imani ya kuwa kuna uhai baada ya kifo, kuendeleza umoja na ushirikiano, kuonya na kukosoa mwenendo wa jamii, kuelimisha, kuelezea matatizo ya jamii na utatuzi wake na kujipatia kipato kwa watendaji wa mbolezi. Kwa hiyo, makala hii inajadili dhima mbalimbali za mbolezi katika jamii ya Wakinga mbali na dhima iliyozoeleka ya kuliwaza. Dhima hizo zimepatikana kwa kutumia mbinu mbalimbali katika ukusanyaji wa data, badala ya kuchambua mashairi ya mbolezi pekee.

## 1.0 Utangulizi

Mbolezi zimefasiliwa kama ushairi unaohusu kifo (Okpewho, 1992; Ojaide, 2005), nyimbo za misiba na maafa (Mulokozi, 1996) au nyimbo zinazotumika kwenye maombolezo (Finnegan, 2017). Mbolezi ni fani muhimu katika shughuli za msiba kote barani Afrika (Okpewho, 1992; Ojaide, 2005; Finnegan, 2017) na hakuna kifo kisichoambatana na mbolezi. Okpewho (1992) anaeleza kuwa Afrika ya Magharibi, mbolezi huambatana na tambiko maalumu kuhusu kifo. Naye Kidane (2012) katika utafiti wake wa mbolezi katika jamii ya Kaficho nchini Ethiopia amebaini kuwa kuna aina tatu za mbolezi: *shoosho* (mbolezi zinazoimbwa na kutendwa na mtu yeyote yule bila kujali jinsi yake), *hicho* (mbolezi zinazoimbwa na kutendwa na wanaume) na *gommo* (mbolezi zinazoimbwa na kutendwa na wanawake).

Katika tamaduni nyingi za jamii za Kiafrika, hakuna tofauti dhahiri kati ya maisha ya ulimwengu unaoonekana na ulimwengu usioonekana ambako ni hatima ya maisha ya mwanadamu (Mbiti, 1969). Kwa hiyo, kifo hakitazamwi kama mwisho wa maisha ya binadamu, bali ni mwendelezo wa maisha baada ya kifo.

*Kioo cha Lugha 2020, 18: 208-228*

Kutokana na kutoepukika kwa kifo na imani kuhusu maisha baada ya kifo katika tamaduni za Afrika, ikiwamo Tanzania, jamii mbalimbali zimejiwekea taratibu za kijamii ili kupunguza majonzi ya kuondokewa na mpendwa wao. Taratibu hufanyika kumsindikiza marehemu kuingia katika ulimwengu mwingine ili aishi na wazee waliotangulia au kufika salama huko aendako. Mambo kadhaa huathiri namna jamii inavyopokea majonzi ya kuondokewa na mpendwa wao. Mambo hayo ni uelewa wa maana ya kifo, uhusiano kati ya mtu aliyekufa na waliohai, aina ya kifo na mtandao wa uhusiano walionao wafiwa (Platt na Persico, 1992). Kwa jumla, mambo haya pia hutofautisha namna jamii zenye tamaduni mbalimbali zinavyochukulia suala la kifo na shughuli zinazoambatana na maziko (McCaskie, 1989).

Uchache wa tafiti za kifasihi zinazochunguza mbolezi umechangia kwa kiasi kikubwa kutokufahamika kwa dhima zake miongoni mwa jamii mbalimbali. Baadhi ya watafiti wameeleza kuwa kama ilivyo kwa kazi za fasihi, katika kumulika hatua mbalimbali za maisha ya mwanadamu, mbolezi hutoa mwanga kuhusu kifo kwa wasikilizaji na watazamaji wake (Hakola na Kivistö, 2014). Hivyo, mbolezi hutumiwa kama nyenzo ya kuunda masimulizi yanayohusu kifo, ili kujenga hisia na kuibua mitazamo na tafakuri mbalimbali kuhusu maisha ya hapa duniani, kifo na maisha baada ya kifo. Hokona na Kivistö (khj) wanaeleza kuwa baadhi ya tanzu za fasihi zinaandikwa maalumu kwa ajili ya kuonesha hisia ya kuondokewa na mpendwa, hivyo fasihi iliyobebwa kwenye tanzu hizo ikiwamo mbolezi hutumika kuliwaza waliofikwa na majonzi. Pamoja na watafiti kudokeza kuwapo kwa mbolezi, baadhi yao kama vile Finnegan (2012) wanaonesha kuwa kipera cha mbolezi hakiko bayana katika jamii za Kiafrika na hata kikijitokeza hakina tukio maalumu.

Nchini Tanzania, utafiti ulioangazia mbolezi umefanywa katika makabila machache na umejikita zaidi kutazama dhamira ya mbolezi kwa kuchambua mashairi ya nyimbo zinazoimbwa msibani (Amanyisye, 2017). Aidha, tafiti hizo zinatumia mbinu chache katika kukusanya data na zinakosa matumizi ya nadharia katika uchambuzi wa data hizo ili kuongoza uelewa wa mbolezi kwa kina. Mulokozi anaeleza kuwa wataalamu wengi wanajadili dhima za fasihi pasipokutumia nadharia maalumu, hivyo kuzorotesha uwezekano wa kujadili dhima za mbolezi kwa kina (Mulokozi, 2017). Anaongeza kuwa wakati wa uchambuzi itikadi na utabaka hujitokeza kwa namna tofautitofauti. Kazi yoyote ya fasihi (zikiwamo mbolezi) ni lazima ziwe na dhima ya kiitikadi, kiuchumi, kiutamaduni, kisiasa, kifalsafa na kiujumi. Mulokozi (khj) anajumuisha kuwa dhima ya jumla ya kazi ya fasihi ni kusawiri kisanaa hali ya mwanadamu, mazingira yake, uhusiano wake na mazingira hayo, mahusiano yake na jamii, hisia na mawazo yake, kwa lengo la kuelewesha, kubadilisha, au kwa lengo la kuonesha hali ilivyo. Makala hii

imeonesha hali ilivyo katika jamii ya Wakinga kwa kutumia Nadharia ya Ontolojia ya Kibantu.

## 2.0 Nadharia ya Ontolojia ya Kibantu

Utafiti unaojenga makala hii uliongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kibantu. Nadharia hii iliasisiwa na Tempels (1959) ambayo aliielezea kuwa ni mtazamo unaohusu chanzo na kuwapo kwa kila kiumbe na uhusiano wake katika jamii za Wabantu. Katika nadharia hii familia inatazamwa kwa mapana zaidi, kwani hujumuisha waliohai na wafu (ambao hutambulika kama mizimu). Aidha, nadharia hii inatambua kuwapo kwa Mungu Mkuu na muumbaji ambaye ndiye chanzo cha kani uhai. Katika uhusiano huu, watu waliohai wamepewa mamlaka ya kutawala viumbe vyote. Kila kiumbe kina kani uhai ambayo hutolewa na Mungu Mkuu. Hivyo, katika kuelezea mahusiano yaliyopo kati ya waliohai, wafu na vitu, Tempels anasema waanzilishi wa kila ukoo, wako karibu sana na Mungu; hawaitwi wafu bali hujulikana kwa jina la '*ba-Vidye*' (viumbe hai endelevu). Hao wanaelezwa kuwa wapo kwa ajili ya Mungu na ni waimarishaji wa kwanza wa uhai kwa kila ukoo na ni wawezeshaji wa uhai kwa watu waliomo duniani.

Katika utafiti wake Tempels (khj) aligundua kuwa jamii ya Waluba ilitofautisha kati ya wahenga ('*ba-tata*') au ('*Ba-nkambo*') katika mtiririko wa wahenga na wafu ('*Bafu*'). Wafu waliwekwa katika kundi la watu wa kawaida, hawakuwa viongozi wa ukoo. Hali kadhalika mfu (mzimu) anayesababisha mabaya duniani, huwa hakumbukwi kabisa. Utaratibu hufanywa ili kumtenganisha na waliohai; na humsindikiza kuelekea katika ulimwengu wa waliolaaniwa (Tempels, 1959).

Utafiti uliofanywa takribani muongo mmoja baada ya Temples, ulionesha kuwa Wabantu wana ontolojia yao inayofuata imani yao. Katika ontolojia ya Kibantu, watu waliohai wanaaminiwa kuwa na uhusiano mkubwa na wafu (mizimu) na wahenga ambako ndiko kikomo cha maisha yake (Mbiti, 1969). Pia, Mbiti (khj) anaeleza kuwa, mizimu hutumiwa na Waafrika kama daraja katika kuwaunganisha walio katika ulimwengu unaoonekana na Mungu katika masuala ya ibada. Waafrika wanaamini kuwa wakitumia mizimu katika ibada zao wanajibiwa haraka kwa sababu mizimu inajua lugha ya ulimwengu unaoonekana na usioonekana. Aidha, Mbiti (khj) anabainisha kuwa ontolojia ya Wabantu imegawanywa katika darajia tano. Darajia hizo tano zinaonekana kuwa na uhusiano na mwanadamu hai na ndiye anayetegemewa kuimarisha mahusiano hayo. Mosi, ni darajia ya Mungu ambaye ndiye mwanzilishi wa mwanadamu na kila kitu kinachoonekana na kisichoonekana na ndiye anayewezesha uhai wa vitu vyote akiwamo mwanadamu. Darajia ya pili ni roho ambayo ni kikomo au hatima ya mwanadamu hai – baada ya kufa hubadilika na kuwa roho bila mwili. Darajia ya tatu ni mwanadamu, ndiye kitovu cha ontolojia,

ndiye mchagizaji wa darajia zingine. Nne, ni darajia ya wanyama na mimea ambayo mwanadamu huwezeshwa na mimea kuishi na wanyama ni kitoweo kwake na hao wanyama hutumika katika masuala ya kiibada. Darajia ya mwisho ni viumbe visivyohai, huambatana na mazingira ambamo mwanadamu anaishi na mwanadamu huendeleza mahusiano yake na mazingira hayo (Mbiti, 1969).

Akichangia mjadala wa Nadharia ya Ontolojia, Mulokozi (2017) anaeleza kuwa ontolojia ni maarifa, mtazamo na imani ya jamii kuhusu maisha na kuwapo kwake na kuhusu ulimwengu kwa jumla. Kwa mtazamo wake, ontolojia ni zao la maswali ya mwanadamu kuhusu kuwepo kwake. Maswali hayo ni kama vile: binadamu ni nani? Asili ya binadamu ni nini? Asili ya mwanaume au mwanamke ni nini? Asili ya ulimwengu ni nini? Lengo na hatima ya maisha ni nini? Je, kuna mamlaka au nguvu nje ya ulimwengu inayotawala maisha ya mwanadamu? Binadamu anahusiana vipi na ulimwengu na vitu vilivyomo? Mauti ni nini? Je, kuna maisha baada ya kufa? Halikadhalika, Mulokozi (khj) anaainisha vipengele mbalimbali vinavyoweza kutumika kama mwongozo katika kuhakiki kazi za kifasihi ili kuielewa ontolojia ya Kibantu. Mambo hayo ni: Mosi, dhana ya familia pana, kuwepo kwa familia inayoishi sasa, waliokufa na ambao hawajazaliwa. Pili, kuheshimu wahenga kwa njia ya kufanya matambiko. Tatu, kuthamini uzazi – yaani imani kuwa mwanadamu akikosa uzao ni laana. Nne, imani katika sihiri na uchawi – imani kuwa kila baya na kifo vinatokana na uchawi. Tano, umoja, mshikamano na mkamilishano wa maumbile na vilivyomo – ikimaanisha kuwa ukamilifu wa mtu mmoja unatokana na kuwapo kwa mtu mwingine au mizimu au vitu vinavyomzunguka. Sita, uanthropomofia – imani ya kumtanguliza mwanadamu katika masuala ya imani, miviga, mizimu, miungu n.k. Inajumuisha namna ya kumhudumia mwanadamu awapo hapa duniani. Urquizer na Kotrschal (2015) wanaeleza kuwa athropomofia ni utoaji wa sifa au tabia ya ubinadamu kwa kitu ambacho si binadamu katika mazingira yanayomzunguka mwanadamu. Sifa au tabia hizo hutokana na mawazo au hisia alizonazo mwanadamu juu ya vitu vinavyomzunguka.

Imani kuhusu binadamu, uhusiano na ushirikiano wa binadamu waliohai na wafu, uhusiano wa binadamu hai, mazingira na vitu vinavyomzunguka, ni baadhi ya mambo yanayoweza kutoa mwanga kuhusu dhima za mbolezi. Hata hivyo, kuna ombwe la utafiti unaoangazia dhima za mbolezi nchini Tanzania. Makala hii imeangazia dhima ya mbolezi za sasa za Wakinga wanaoishi wilayani Makete mkoani Njombe kwa kuchunguza mbolezi zinazotendwa msibani. Makala imehoji watunzi, waimbaji na wakazi wa vijiji mbalimbali wilayani Makete ili kuelewa kwa kina dhima ya mbolezi kama zinavyoelezwa na wahusika wenyewe.

## 3.0 Mbinu Zilizotumika Kukusanya na Kuchambua Data

Makala hii ni zao la utafiti uliofanyika katika jamii ya Wakinga wanaoishi wilayani Makete, mkoani Njombe. Vijiji husika vilichaguliwa kwa kuzingatia usampulishaji wa madhumuni maalumu ili kupata vile visivyo na mwingiliano mkubwa na wageni na vyenye mwingiliano na wageni katika kata zilizopo wilayani humo. Uchaguzi huu ulishirikisha viongozi wa kata husika na viongozi wa kimila. Hivyo, vijiji vya Ivalalila (kata ya Iwawa), Bulongwa (kata ya Bulongwa), Maliwa (kata ya Ipepo) na Lupila (kata ya Lupila) vilihusishwa katika kupata data. Wadau walioshirikishwa katika utafiti ni pamoja na watendaji wa mbolezi, viongozi wa kimila na wakazi katika vijiji husika. Uchaguzi wa watoa taarifa ulizingatia mbinu ya usampulishaji wa madhumuni maalumu na usampulishaji tajwa, ili kufikia malengo ya utafiti. Wakazi wa vijiji husika walishiriki katika majadiliano ya makundi lengwa yenye washiriki kati ya 6 mpaka 8 kwa kila kundi na kufanya jumla ya makundi kumi na sita (16) kwa vijiji vyote vinne. Aidha, jumla ya washiriki 48 walishiriki kwenye mahojiano. Maswali yaliyoulizwa katika makundi lengwa yalilenga kupata mtazamo wa jumla kuhusu mbolezi na dhima zake, wakati mahojiano na watu mahsusi yalilenga kupata mtazamo wa mtu mmoja mmoja kulingana na uhusika wake katika utendaji wa mbolezi miongoni mwa Wakinga. Mbinu yingine iliyotumika ni ushuhudiaji wa kushiriki. Mtafiti alishuhudia na kushiriki katika matukio yanayosababisha mbolezi kutendwa na kujua dhima za utendaji wake. Aidha kutokana na kutopata misiba toshelevu utafiti huu ulitumia mbinu ya uchambuzi wa matini zilizorekodiwa.

Kutokana na aina ya data, uchambuzi wa data ulikuwa wa kitaamuli. Programu ya ngamizi iitwayo *Maxqda* ilitumika kupanga data katika misimbo ili kurahisisha udondozi wa data kutoka katika mbolezi husika na zile zilizopatikana kutoka kwa washiriki wa utafiti katika makundi lengwa, mahojiano na ushuhudiaji wa kushiriki katika vijiji husika. Data hizo ziliwekwa katika misimbo, kisha kuchambuliwa kwa kuzingatia lengo mahususi la utafiti ambalo ni dhima ya mbolezi katika jamii ya Wakinga. Aidha, lengo hili limechambuliwa kwa kutumia Nadharia ya Ontolojia ya Kibantu.

## 4.0 Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inachambua na kujadili data za utafiti. Hata hivyo, ili kufanya mjadala huo ueleweke kwa urahisi kwa wasomaji wa makala hii, kwanza tunabainisha mazingira halisi ya msiba miongoni mwa Wakinga. Mazingira haya yalibainika wakati tunafanya ushuhudiaji wa kushiriki katika misiba kwenye eneo la utafiti.

### 4.1 Mazingira ya Msiba katika Jamii ya Wakinga

Katika jamii ya Wakinga, msiba unapotokea, wafiwa wa familia iliyofikwa na

msiba hujawa na huzuni ya kuondokewa na mpendwa wao. Huzuni hiyo huambatana na vilio na kelele za huzuni ambazo aghalabu huwavuta majirani na wapita njia kuja kuungana na wafiwa ili kuomboleza msiba ulioifika familia husika. Yeyote anayekuja eneo la msiba huangua kilio. Vilio hivyo ndivyo huwavuta watu wengine na kutambulisha kuwapo wa msiba katika familia husika.

Zipo njia zingine mbalimbali zinazotumiwa kuwajulisha watu wa vijiji vya jirani kuhusu msiba. Njia mojawapo ni kupiga kelele maalumu zinazoashiria msiba ambapo mpigaji husimama juu ya mlima. Mtu huyo anapopiga kelele hizo hutaja jina la marehemu na jina la ukoo uliopatwa na msiba. Njia ya pili ambayo ni maarufu ni kutumia mbiu inayopigwa kwa kutumia pembe ya mnyama aitwaye paa. Pembe hiyo (taz. picha namba 1 na 2) kwa lugha ya Kikinga huitwa *lukelema*. Mpiga-mbiu husimama juu ya kilima kinachoelekea vijiji jirani ili mvumo wa mbiu uweze kufika katika vijiji hivyo.

**Picha Na. 1 & 2: Mpiga-mbiu ameshika *lukelema* ipigwayo kuashiria msiba**



**Chanzo:** Mtafiti, kijiji cha Maliwa (2017)

Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya sasa yanayohusisha mwingiliano wa imani, si misiba yote ambayo *lukelema* hutumiwa. Endapo marehemu ni muumini wa dini ya Kikristo, waombolezaji huitwa kwa kupiga kengele kanisani alikokuwa akiabudu. Kengele hii hupigwa kwa vituo vya miimbo mitatu-mitatu na kupumzika kwa dakika kadhaa na kuendelea. Namna hii ya upigaji kengele huashiria kuwapo kwa msiba. Baada ya utoaji wa taarifa kwa njia hizo tofauti, wanajamii huanza kukusanyika eneo la msiba. Huanza kuomboleza kwa mbolezi kulingana na imani ya marehemu. Zifuatazo ni dhima za mbolezi kwa mujibu wa utafiti huu.

### 4.2 Dhima za Mbolezi

Mbolezi zina dhima mbalimbali. Baadhi ya dhima hizo kwa mujibu wa makala hii ni kuliwaza, kutunza na kuendeleza amali za jamii, kuelimisha, kuelezea hali ya jamii, kuonya na kukosoa na kujipatia kipato miongoni mwa watendaji wa mbolezi hizo.

### 4.2.1 Kuliwaza Wafiwa

Kuliwaza ni dhima iliyojadiliwa kwa kina katika makundi lengwa na mahojiano ya kina na washiriki wote waliowezesha kupata data ya uandishi wa makala hii. Mathalani, washiriki walieleza kuwa nyimbo au maneno yanayotamkwa wakati wa msiba hulenga "kumsaidia mtu aliyefikwa na msiba ajisikie vizuri" au "ili mfiwa asiumie zaidi kutokana na huzuni anayopitia". Kwa sababu hiyo, nyimbo zinazolenga kuliwaza huambatana na tumaini kwamba ipo siku ambayo wafiwa wataonana na ndugu yao aliyeondoka[1]. Maana halisi ya kuondoka (kufa) kwa Wakinga ni safari na ndiyo maana miili ya hao walioondoka huhifadhiwa mahali maalumu panapoitwa "*kumahame" au* mahameni kama ishara kuwa ndugu wote wanapaswa kukusanyika sehemu hiyo. Kwa hiyo, mbolezi-nyimbo (hutendwa na watu waliokuja kuhani pamoja na ndugu) na mbolezi-maghani (hughanwa zaidi na wafiwa) hutumika kukumbushana na kuwakumbusha wafiwa kuwa hakuna haja ya kuhuzunika wala kulia sana. Kwa sababu kila mtu ataondoka na kukutana na wapendwa waliotangulia katika safari hiyo. Mshiriki katika kundi lengwa katika kijiji cha Ivalalila, anasema:

> Mimi ndipo ninapoelewa hapo kwamba, kazi kubwa ya hizi nyimbo ni kumfariji yule mfiwa kwa sababu kuna siku wataonana na aliyeondoka, na kwamba hii safari si ya mtu mmoja ila ni yetu wote. (Mahojiano, Ivalalila, tar 22.07.2017)

Mbolezi hutendwa na watu waliofika msibani au na wafiwa wenyewe katika jamii ya Wakinga. Washiriki katika makundi lengwa na mahojiano walibainisha kuwa, watu wanaofika msibani hutenda mbolezi-nyimbo au mbolezi-maghani. Lengo ni kuwakumbusha wafiwa maana halisi ya maisha ya hapa duniani kuwa ni safari na kuwa mtu aliyekufa ametangulia kufanya safari hiyo ambayo wote ndiko wanakoelekea. Pia, wafiwa wanapozitenda mbolezi hulenga kujifariji au kufarijiana wao kwa wao.

Kwa hiyo, kuliwaza ni suala la mjadala. Kuliwazika kunategemea ukaribu wa mfiwa na marehemu aliyefariki. Endapo aliyefariki alikuwa ni tegemeo kubwa kiuchumi huwa wafiwa inawachukua muda mrefu kufarijika na kusahau. Aidha, kama marehemu hakuwa tegemeo kubwa kiuchumi, huwa kuliwazika kunachukua muda mfupi kwa mujibu wa maelezo ya wahojiwa.

### 4.2.2 Kuendeleza Imani kuwa kuna Uhai baada ya Kifo

Utafiti huu umechunguza mbolezi katika jamii ya Wakinga jinsi zinavyotendwa kwa

[1] Katika utafiti huu, washiriki walizungumzia zaidi "kuondoka" na si kufa au kufariki.

kuambatana na imani juu ya uwapo wa uhai baada ya kifo. Katika mahojiano, majadiliano na ushuhudiaji wa kushiriki, watoa taarifa wanasema kuwa kwa asili Wakinga wanaamini kuwa mtu akifa mwisho wa safari yake ni mahameni (*kumahame*). Huko mahameni anaenda kuishi pamoja na wazee wake au ndugu zake waliokufa zamani, sawa na Tempels aliposema ‘roho ndiyo ukomo wa mwanadamu’ (Tempels, 1959). Watoa taarifa wanaeleza kuwa mahameni ni mahali ambapo kila ndugu wa ukoo anapofariki, lazima roho yake ipelekwe hapo kwa matendo maalumu ya kimila yanayoambatana na tambiko. Watendaji wa tambiko hutenda vitendo ambavyo huambatana na maneno maalumu ambayo yana sifa ya maghani. Kisha hufurahi kwa kuimba mbolezi-nyimbo na kucheza ngoma za asili za Kikinga. Katika utaratibu huu ni jambo gumu kutenganisha matendo dhati na matendo ya kisanaa (fasihi).

Jamii ya Wakinga wanaamini kuwa hata kama mtu atakufa na kuzikwa mahali pengine, utaratibu hufanywa ili kuihamisha[2] roho ya marehemu. Huizika tena kwenye kaburi dogo linaloandaliwa mahali ambapo watu wote wa ukoo wake huzikwa. Katika muktadha huu, hatima ya maisha ya Wakinga siyo pale ulipozikwa mwili, bali ni mahali inapopelekwa roho baada ya uhamisho (*kutekela*). Wakinga wanaamini kuwa uhamisho wa roho ya marehemu kwenda mahameni unapokamilika, ndipo waliohai pamoja na wafu huwa salama. Jambo hili lilibainishwa pia na Tempels (1959) kuwa kuna mizimu ambayo huwadhuru watu, mpaka ifungwe ndipo hali huwa salama. Pia, Mbiti (1991) anaeleza kuwa endapo taratibu zisipofuatwa katika mazishi kuna baadhi ya mizimu huweza kugeuka na kuwadhuru wanadamu waliohai. Wakinga wanapofanya mchakato wa uhamisho wa roho za wafu huambatana na mbolezi-maghani kwa kutamka baadhi ya maneno. Wakishamaliza kumhifadhi mahameni, husherehekea kwa kunywa pombe na kutenda mbolezi-nyimbo.

Maneno ya mbolezi-maghani ambayo yanaghanwa na wafiwa wakati wa misiba yanadhihirisha kuwa ndugu waliokufa wako katika kusanyiko moja na wanakutana. Mathalani, katika msiba wa mtoto tulioushuhudia katika kijiji cha Maliwa tarehe 27/08/2017, maneno ya mbolezi-maghani yaliyoghanwa na wafiwa yalihusisha kutuma salamu kwa waliotangulia, akiwamo baba yake marehemu. Walisema ‘*Vasamtsyake voni*’ (Uwasalimie wote), *Ukamsamtsyake nu dadajo*’ (Ukamsalimie na baba yako). Aidha, tulimshuhudia mghani mwingine katika kijiji cha Ivalalila, tarehe 24/07/2017 akisema ‘*Uve Magareti ukavasamtsyake voni, ukavasamtsyake voni, voni voni*’ (*Wewe Magareti ukawasalimie wote, ukawasalimie wote, wote wote*). Maana yake ni kwamba Magareti aende akawasalimie wote

[2] Hufanywa kwa kutamka maneno maalumu ambayo yana sifa ya maghani.

waliokwisha fariki. Hivyo, ni dhahiri kuwa salamu zinazotumwa zinaenda kwa wale waliokufa miaka ya nyuma. Pia, wanaamini kuwa wanaokufa huwa wanaendelea kuwa hai katika mfumo mwingine wa maisha kama anavyoeleza Mbiti (1969; 1991). Hivyo, kwa imani ya Wakinga hakuna ukomo wa uhai lakini kuna ukomo wa safari ya roho ambapo huhifadhiwa mahameni na huendeleza mahusiano kwa utaratibu maalumu.

Mbali na mbolezi-maghani, pia waombolezaji kupitia mbolezi-nyimbo wanathibitisha kuwa kuna uhai baada ya kifo. Ndiyo maana wanaendeleza na kutunza mila na desturi katika mahame ya Wakinga. Ufuatao ni mbolezi-wimbo ulioimbwa wakati wa msiba huko Lupila:

| | |
|---|---|
| (1) *Uve Marehemu* | Wewe Marehemu |
| Kikinga | Kiswahili |
| 1. *Uve marehemu linga ukavonake kununu vise un'ole,* | 1. Wewe marehemu ukiona huko kuzuri uje unichukue, |
| 2. *Linga ukavonake kuvivi utamake kuko* | 2. Ukiona kubaya ubaki hukohuko |

**Chanzo:** Data ya Uwandani, kijiji cha Lupila (2017) (Tafsiri yetu[3])

Wimbo huu unadhihirisha uhai endelevu wa mtu aliyekufa. Pia, mbali na kuwa hai anahusishwa na kutambua uzuri na ubaya wa mambo yanayomzunguka. Hivyo jamii hii inaamini uhai baada ya kifo na kuna umuhimu wa kuwahifadhi na kuwahudumia vema wafu.

Kutokana na mwingiliano wa imani, kuna baadhi ya Wakinga ambao wanaamini katika Ukristo. Wanaeleza kuwa kwa imani yao mtu akifa huwa amelala anangoja hadi siku ya ufufuo. Wafu watafufuliwa kwanza na kisha kuambatana na waliohai na kusubiri hukumu kutokana na matendo waliyotenda duniani. Wakristo waliohojiwa wanaeleza kuwa hatima ya roho ya mtu akifa inategemea matendo yake akiwa hai. Mathalani, endapo marehemu alitenda mabaya wanaamini kuwa atatupwa kwenye ziwa la moto, na endapo alitenda mema ataishi milele. Hivyo, Wakinga wa imani za asili na Wakinga Wakristo wanaamini kuwapo kwa maisha baada ya kifo mahameni ama mbinguni. Pia, wanaamini katika umilele. Mbolezi-nyimbo zinazopatikana katika jamii hii, ni nyimbo zilizo katika lugha ya Kikinga, Kiswahili na nyimbo za jamii-lugha jirani kama vile Wabena na Wanyakyusa. Ufuatao ni wimbo unaoashiria tumaini la waumini wa Kikristo juu ya wafu:

[3] Kila mbolezi iliyo katika lugha ya Kikinga imetafsiriwa kwenda lugha ya Kiswahili kwa ushirikiano kati ya mtafiti na watafiti wasaidizi

(2) Haleluya Tutaonana

1. Haleluya tutaonana
2. Haleluya tutaonana,
3. Tutaonana mbinguni kwa baba
4. Haleluya tutaonana.

**Chanzo:** Data ya Uwandani, kijiji cha Ivalalila (2017)

Katika wimbo huu waimbaji wanaeleza kuwa kuna tumaini la kuonana tena na marehemu. Kutokana na misingi ya imani ya Kikristo kuonana huko ni mahali panapoitwa mbinguni ambako yuko baba wa waumini wote wa imani ya Wakristo. Hivyo, kwa imani hii pia kuna uhai baada ya kifo ila ni uhai ambao ni roho.

Aidha, kwa upande mwingine inaelezwa kuwa kutowahifadhi marehemu mahameni na kutowahudumia kunaweza kuleta matatizo kadhaa kwa jamii. Matataizo hayo ni pamoja na kutangatanga kwa mizimu ambayo huweza kuchukia na kuleta matatizo kwa ndugu zao waliobaki duniani. Matatizo mengine ni kuleta magonjwa yasiyokuwa na tiba, migogoro na ugomvi usioisha katika familia, hasara katika shughuli za kiuchumi (kama vile kilimo na biashara), kuvuruga ndoa, kuzuia watoto wasifanikiwe kwenye masomo yao, n.k. Mhojiwa mmojawapo alikuwa na haya ya kusema:

> ...kwa mila unaweza ukaona tunalima shamba tuko pamoja, mimi shamba liko katikati huku shamba la mwenzangu huku shamba la mwenzangu. Mimi shamba langu litaliwa na ndege lote, mwenzangu tuliyepakana halijaliwa. Sasa utajiuliza kwa nini hawa ndege wanashambulia shamba langu tu? Mbona wenzangu hawapati shida? Kwa hiyo ukitembea utaona kumbe *source* ni hii.

(Mahojiano na Kiongozi wa mila, Maliwa, tar. 26/08/2017)

Hapa mhojiwa anaamini mizimu ndiyo inayomletea hasara. Suala hili limeelezwa pia na Mbiti (1991) alipokuwa anabainisha aina za roho, anasema kwamba roho zinazotokana na wanadamu yaani mizimu huwa zinaweza kugeuka na kuja kuwadhuru wanadamu kwa kuwaletea magonjwa, mikosi na hata kusababisha mauti. Hivyo, Wakinga wengi wanaofuata mambo ya asili wanachoogopa ni athari hasi inayotokana na kutowahifadhi marehemu mahameni na kutowahudumia wafu. Hivyo matendo haya ya kimila hufanywa huku yakiambatana na mbolezi-maghani na mbolezi-nyimbo ili kuepukana na changamoto hizo.

Katika mahojiano na wazee, mwanamke mmoja pia alieleza madhara yanayoweza kutokea kwa kutomfunga marehemu na kumuweka mahali pa ukoo. Anasema yafuatayo:

> Utakuta watoto wanapata madhara. Mtoto anakuwa mgonjwa anapata

> homa kali. Mnaanza kujiuliza jamani kwa nini mwanangu anaumwa, au kwa nini mwenzangu anaumwa? Hapo ndipo tunapoenda kwenye utafiti (kwa waganga kuagua). Unaenda kusikiliza, ndipo watakuambia, nenda ukachukue mbuzi uende ukapeleke sehemu kwenye msitu fulani. Ndipo unaenda kupeleka.
> (Mahojiano Maliwa, tar. 25/08/2017)

Nukuu hii inadhihirisha kuwa kinachowasukuma Wakinga kufanya tambiko la uhamisho wa wafu kutoka mahali wanapozikwa kawaida na kwenda mahameni ni hofu inayotokana na mizimu katika familia. Kwa kuwa ni masuala ya imani, wengi wanasema kuwa wakifuata utaratibu huo hawapati shida tena. Kama shida ikijirudia huwa wanaenda tena kwa *Wasung'wa* (waganga) kuagua ili kujua kitu ambacho mizimu wanakitaka kwa wakati huo. Suala la kuhamisha marehemu na kumpeleka mahameni bado linafanywa mpaka wakati huu. Hata baadhi ya Wakinga ambao wamefuata imani ya Kikristo bado wanachanganya na imani hii ya asili kwa kuendelea kuhamisha ndugu zao ili wasipate hasara ya kusumbuliwa na mizimu. Tempels (1959) anaeleza kuwa hili ni suala gumu na haliwezi kuthibitishwa kwa sayansi za Kimagharibi, ni maisha ya Waafrika na ni halisi. Imani ya kuhamishia wafu mahameni ndiyo inayowafanya wenyeji waendelee kuenzi taratibu hizo za asili juu ya wafu, zinazoambatana na mbolezi-nyimbo na mbolezi-maghani ambayo yanadhihirisha kuwa ndugu zao bado wako hai mahameni na wao wakifa watakutana nao.

### 4.2.3 Kuendeleza Umoja na Ushirikiano

Umoja na ushirikiano katika jamii ya Wakinga upo kati ya waliohai kwa waliohai, na kati ya wafu na waliohai. Ushirikano na waliohai hujidhihirisha nyakati za misiba na matukio mengine ya kijamii. Mtu asiposhiriki huweza kupewa adhabu fulani na kutoimbiwa, wakazika tu na kutawanyika bila kurudi tena nyumbani kwa ajili ya kuwafariji kwa mbolezi-nyimbo. Wimbo ufuatao unadhihirisha hilo:

| (3) *Une Nuve* | Mimi Nawe |
|---|---|
| Kikinga | Kiswahili |
| 1. *Une nuve x3* | 1. Mimi nawe x3 |
| 2. *Haki ya Mungu tulivapina twe voni* | 2. Haki ya Mungu sisi sote ni wakiwa |

**Chanzo:** Data ya Uwandani, kijiji cha Maliwa (2017)

Wimbo huu unahimiza suala la ushirika kati ya watu walioondokewa na wazazi wao. Inaelezwa kwamba kwa kuwa sote ni wakiwa, inabidi tujaliane na kusaidiana; tusitengane. Watendaji wanataka watu wawe na umoja hasa katika masuala ya matatizo. Wimbo ufuatao pia unabainisha dhima ya umoja:

| (4) *Twimile Twilola* | Tumesimama Tunaona |
|---|---|
| Kikinga | Kiswahili |
| 1. *Twimile twilola x3* | 1. Tumesimama tunaona x3 |
| 2. *Kilavo na mtondo utuvonage* | 2. Kesho na keshokutwa ukatuone pia |

**Chanzo:** Data ya Uwandani, kijiji cha Maliwa (2017)

Wanajamii wanataka kila mmoja ashiriki shughuli za kila siku za jamii. Mbali na kwamba kuna ushirika na umoja kati ya waliokufa na wafu pia wanataka kila mwanajamii aliyehai awe na ushirika kati yao. Katika wimbo huu inaelezwa kuwa unapoona wenzako wamekuja leo msibani kwako, wanaamini kuwa nawe siku wakifiwa utaenda kuwaona na kuwafariji. Ushirikiano ni muhimu kwa sababu wakati wa matatizo mtu hawezi kujisaidia mwenyewe, anahitaji msaada wa wengine katika kufanikisha shughuli nzima ya msiba. Shughuli hizo ni pamoja na kufarijiana kwa maneno, kuchimba kaburi, kupika vyakula, kupokea wageni, kuimba, na kulala matanga. Kama mwanajamii hahudhurii misiba basi siku ya msiba wataweza kumwimbia nyimbo za kumuonya, na wakati mwingine hawamwimbii ili naye awe anatoka kuwaimbia wenzake. Adhabu ya kutomuimbia imeonekana kuzungumzwa zaidi na wanawake kuliko wanaume, kwa madai kuwa kuimba ni sehemu ya kufariji na wanawake ndio huwa wanaumizwa sana na msiba. Hivyo mwanamke asipojitoa kwa wenzake na wao hawafiki kumfariji (Mahojiano katika kijiji cha Bulongwa, Tar 27/07/2017). Ontolojia ya Kibantu inaamini katika umoja (Tempels, 1959; Mbiti, 1991), ndiyo maana katika msiba au shughuli yoyote ikitokea, wanajamii wote huona ni wajibu wao kushiriki kiukamilifu ili kukwepa adhabu ya kulipa pesa pamoja na kuomba msamaha.

Suala la kufariji wakati wa msiba, pia linahusisha waumini wa imani ya Kikristo. Waimbaji wa nyimbo za Kikristo huimba kwa kutegemea utaratibu wa kanisa na imani ya marehemu. Waumini wa kata ya Bulongwa wanaeleza kuwa hawaendi kuimba katika msiba wowote bali huimba kwa mtu ambaye amekwishakuwa muumini wa imani hiyo (Mahojiano Bulongwa Tar. 25/07/2017). Hii ni tofauti na wahojiwa wa kata ya Ipepo na Lupila ambao huimba kwa kila msiba. Pia, kama si muumini wa imani ya Kikristo hawajitokezi kuimba kabisa. Hii ni mbinu inayotumika ili kuwafanya wale wasioamini Ukristo wajisikie vibaya na hatimaye wabadili imani zao na kufuata Ukristo. Hali kadhalika waumini na wasio Wakristo hutengwa hata katika kuzika: kuna makaburi ya wapagani na wanaomwamini Yesu Kristo. Suala hili limezungumziwa pia na Pagalo (1996) kuwa muumini akikutwa na hatia pengine amekiuka baadhi ya misingi ya imani ya Kikristo anatengwa na kanisa na akifa hazikwi na kanisa.

Aidha, waimbaji wa mbolezi-nyimbo za asili ambazo si za dini ya Kikristo,

wanaimba kwa wanajamii wote bila kujali kuwa ni Mkristo au la ilimradi wapewe nafasi, ingawa ubaguzi kutoka imani ya Kikristo katika baadhi ya kata, hasa ya Bulongwa, umebainishwa katika mahojiano yetu na watoa taarifa. Wasiofuata imani ya Ukristo wanaonekana kuwa wana dhambi na nyimbo zao kuonekana hazileti amani katika misiba yao. Aidha, wasiofuata imani ya Ukristo wanashutumiwa kwa kuleta machafuko kwa sababu nyimbo zao kuna wakati zinauliza nani amemuua ndugu yangu (‘*Uveni abudile ujuva?*’). Kwa hiyo, wanaoamini Ukristo wanaona kuwa kuuliza swali kama hilo ni kutiliana mashaka na kunaweza kuleta ugomvi katika jamii.

Hata hivyo, umoja kwa Wakinga hauishii kwa watu waliohai pekee, bali pia kati ya watu waliohai na wafu. Umoja huo hudhihirika kupitia imani kwamba waliofariki huwawezesha waliohai kuishi salama na kuwafanikisha katika maisha yao ya kila siku. Waliohai jukumu lao ni kwenda kufanya ibada kwa waliokufa ili wawasaidie, pia huwa wanaenda kuwapa chakula na kuwatuliza kama wamechukia. Katika mahojiano mtoataarifa alibainisha yafuatayo:

> Umuhimu upo, kwa sababu nina imani kwamba tukisema tuache ni kitu kisichowezekana, kwa sababu ile mizimu itatudai, itatubana kwa sababu tumeitelekeza. Ndiyo maana inatu*cost* (inatugharimu) kwamba, tuwe tunaenda kusalimia na tunapeleka kuku, tunachinja, tunakula, tunarudi. Kwa sababu wanasema wenzetu katika mila na desturi, watu wa zamani waliamini kwamba, bibi na babu waliofariki ndiyo wanaowalinda na kuwakinga na uchawi. Tusipowakumbuka bibi na babu, ina maana nao watakwepa kutulinda dhidi ya mchawi anayetaka kuja kutuloga. Mchawi atapata nafasi ya kuingia, kwa sababu mila na desturi sizikumbuki, nimezitelekeza. Kwa hiyo matatizo yanaingia.

(Mahojiano, Lupila, tar. 29/08/2017)

Maelezo hayo yanadhihirisha ushirikiano na umoja uliopo kati ya watu waliohai na waliokufa. Maisha ya Mkinga halisi kwa asili yake yamefungamana na wafu. Wafu wanaheshimiwa, wanaabudiwa na wanaamini kuwa wafu wanawapa ulinzi katika kila eneo na kuwafanikisha katika mambo ya uchumi na kuwaepusha na mabaya yote. Hii imebainishwa pia na Mbiti (1991) pale anaposema kuwa Waafrika wanaamini ulimwengu unaoonekana na viumbe vyake na ulimwengu usioonekana na viumbe vyake na wafu wakiwamo.

### 4.2.4 Kuonya na Kukosoa Mwenendo wa Jamii

Mbolezi zina dhima ya kuonya na kukosoa pale ambapo baadhi ya wanajamii hawaendi sawasawa na utaratibu wa jamii waliojiwekea. Suala la kushiriki shughuli

za kijamii ikiwamo misiba ni la lazima, si hiari. Endapo mwanajamii hashiriki misiba basi akifikwa na matatizo wanamuonya kwa maneno na mbolezi. Kwa kutumia mbolezi mtu huweza kuonywa na kukanywa asirudie tena kufanya aliyoyafanya. Pia, mfiwa hukumbushwa kuwa naye anapaswa kushiriki misiba ya wanajamii wengine (rej. Wimbo namba 4 hapo juu). Mashairi ya wimbo huu yanamhimiza mfiwa kushiriki shughuli za misiba kwa wanajamii wenzake. Haya ni maonyo juu ya wanajamii ambao hawashiriki shughuli za msiba katika jamii. Kuonywa huku si kwa kutokufika misibani tu bali pia kwa masuala mengine ya kijamii.

Aidha, maonyo hutolewa kwa watu ambao hawana maadili na hufika wakati jamii humtenga au kumfukuza kabisa. Maadili mabaya ni pamoja na masuala ya uchawi. Wakinga, kama ilivyo kwa Waafrika wengi, wanaamini matatizo mengi katika jamii husababishwa na wachawi. Mpalanzi (2018) anaeleza matatizo hayo ni pamoja na magonjwa, mateso ya kisaikolojia kama vile kumgeuza mtu kuwa mnyama, kunyoa nywele, kukata kucha na hata kifo husababishwa na uchawi. Anaeleza kuwa mandhari ya njia panda na nyakati za usiku hutumiwa na wachawi kuendeleza itikadi za kuuana ama kulipizana visasi. Vivyo hivyo Wakinga wanaamini kuwa kifo cha kijana au mtoto kimesababishwa na uchawi ila mzee akifa ni kawaida kwa sababu umri wake umesonga. Kwa desturi watu wengi ambao hufiwa huwa wanakimbilia kuagua kwa waganga waaguzi (*Vasung'wa*) ili kujua sababu ya kifo cha ndugu yao. Wakishamjua mbaya wao na ikitokea ameumwa, huwa wanamtelekeza. Ikitokea akifariki wanasusia msiba wa mchawi huyo, hawaimbi na hawalali msibani. Mmojawapo wa wahojiwa anaeleza kuwa:

> Babu yangu akawa hana mtu wa kumuuguza. Baba naye alikuwa anagoma kwenda kumchukua, lakini kwa kufuatana na vyombo vya sheria alilazimika kwenda kumchukua. Wakampeleka hospitali ya Ikonda. Watoto wake wengine wakaenda kumchukua kufika Iringa hakumaliza mwezi akafariki. Msiba walirudisha nyumbani (Bulongwa). Hatukuimba kabisa. Kwa sababu ya uchawi wake.

(Majadiliano Bulongwa, tar. 28/07/2017).

Mtoa taarifa anaeleza kuwa adhabu ya mtu asiye mwema hufanyika hata kwa mtu wa karibu kama vile watoto au wajukuu kwa kumsusa mgonjwa. Mtu huadhibiwa tangu akiwa mgonjwa, ndugu humtenga na kuendelea na shughuli zao na hata akifa haombolezewi. Inawezekana kama isingekuwa serikali kuingilia kati huyo babu angesuswa na kuachwa afe bila ya msaada wowote. Hii inaonesha kwamba, suala la uchawi linaikera jamii ya Wakinga, lakini wanashindwa namna ya kulitokomeza. Kwa hiyo, hutumia mbinu ya kuwaonya wakati misiba unapotokea na hasa anapokufa mchawi husika. Ingawa uchawi ni moja ya imani za Kiafrika lakini jamii

ya Wakinga wamekuwa wakiipinga imani hii. Upingaji huu umepata nguvu baada ya ujio wa imani za Kimagharibi, hasa Ukristo ulioingia rasmi kipindi cha ukoloni yaani karne ya kumi na tisa.

Uchawi na athari zake umeelezwa na watafiti wengine, na kwamba suala hili linaathiri kwa kiasi kikubwa maisha ya Waafrika katika maeneo tofauti tofauti ingawa hakuna uthibitisho wa kisayansi. Tempels (1959) anaeleza kuwa mtuhumiwa wa uchawi akihojiwa na kukubali kuwa ametenda, hutekeleza adhabu anayopewa. Naye Mbiti (1991) anaeleza kuwa uchawi ni nguvu ya asili anayokuwa nayo mtu inapotumika vibaya ndiyo hufanya mambo mabaya. Mbiti anakubaliana na Tempels (1959) kuwa kila kifo kwa mtazamo wa Kiafrika kina sababu za kichawi ukiondoa vifo vya wazee ingawa navyo wakati mwingine huhusishwa pia na uchawi.

Kwa kuwa kazi yoyote ya fasihi ni zao la jamii, pia mbolezi-nyimbo za asili na mbolezi-maghani yamebeba ujumbe unaohusiana na kuhoji masuala ya uchawi. Wimbo ufuatao unahoji juu ya nani aliyemuua marehemu:

| (5) *Ikinu Kiki Kyabudile Ujuva* | Kitu Gani Kiliua Mama Yangu |
|---|---|
| Kikinga | Kiswahili |
| 1. *Kivilila kivilila* | 1. Kivilila kivilila |
| 2. *Ikinu kiki ikyabudile ujuva?* | 2. Kitu gani kiliua mama yangu? |
| 3. *Ndiva ndilolile avanjango* | 3. Ninapoangalia wenzangu |
| 4. *Wivitsova nu vanyina* | 4. Wanavyoongea na mama zao |
| 5. *Ndovona Inyihotsi tsikwika tsene* | 5. Huona machozi yatiririka yenyewe |

**Chanzo:** Philip Anyengisye Kusiluka Bulongwa (2017)

Wimbo huu unapoimbwa kwenye msiba wa mwanamke, waimbaji hujaribu kuhoji sababu ya kifo cha marehemu. Kiontolojia Mwafrika anapohoji hivyo maana yake ametilia mashaka kifo cha ndugu yake. Kiimani anaona kuwa hakustahili kufa kwa wakati ule bali amewahishwa na wachawi. Hivyo mbolezi za asili zina nafasi kubwa ya kuhoji masuala ya kiontolojia ya Kibantu katika jamii ya Wakinga kuliko mbolezi-nyimbo za Kikristo.

### 4.2.5 Kuelimisha Jamii

Utafiti huu umebaini kuwa nyimbo za mbolezi hubeba dhima ya kuelimisha jamii juu ya masuala mbalimbali katika jamii, ikiwamo sababu za watu kufa mapema. Elimu inayotolewa na watunzi wa nyimbo hizo ni ile inayolenga kubadili tabia na kuacha ngono zembe, kuchukua tahadhari wakati wa kuuguza wagonjwa, kuwashauri wanandugu kuuguza wagonjwa badala ya kukimbilia kugharamia msiba. *Ndikatsove* (Nikisema) wa Frank Mtulo ni wimbo ambao umekuwa

ukipigwa katika misiba ya jamii ya Wakinga; baadhi ya mistari yake ni kama ifuatayo:

(6) *Ndɨngatsove* [4] Nikisema

| Kikinga | Kiswahili |
|---|---|
| 1. *ʉmunu vʉ ntamu namwilʉta kulola mwe,* | 1. Mtu akiwa mgonjwa hamuendi kumuona nyie, |
| 2. *Mngapʉlɨka aswe po mlʉndamana kʉlonda ɨkalamu nɨ lidaftari,* | 2. Mnasikia amekufa ndio mnakusanyana kutafuta kalamu na daftari, |
| 3. *Gʉtengʉla utsango kunyanakikolo,* | 3. Kuchangisha mchango kwa wanaukoo, |
| 4. *Muhenza nani ɨsisenga mwilya pakɨlɨlo mwe,* | 4. Mnachinja na ng'ombe mnakula kwenye msiba nyie, |
| 5. *Humbe ʉmarehemu aswelye mu nyumba,* | 5. Kumbe marehemu amefia kwenye nyumba, |
| 6. *Mukale mutsange ʉvo bado mwʉmi* | 6. Mngemchangia wakati bado mzima, |
| 7. *Ngalinga (ɨngave) ʉmarehemu ajagye ɨkɨtamu, ɨɨ ɨlelo pʉlɨka.* | 7. Pengine marehemu angepona ugonjwa, leo sikia. |
| 8. *Mngapʉlɨka aswe po mlʉndamana,* | 8. Mkisikia amekufa ndio mnakusanyana, |
| 9. *Avanyakʉlɨla povilela ʉlwihotsi,* | 9. Wanaolia wanalia sana, |
| 10. *Na avanyandalama vileta indalama,* | 10. Na wenye pesa wanaleta pesa, |
| 11. *Ʉkʉgendelela ɨlisanduku ɨlya milioni,* | 11. Kutembelea jeneza la milioni, |
| 12. *Kʉmbe umarihemu jɨbudile ɨnzala,* | 12. Kumbe marehemu amekufa njaa, |
| 13. *Inge wale ntamu mkali ndaku…* | 13. Alipokuwa mgonjwa mlikuwa wapi… |

**Chanzo:** Data ya Maktabani, Wimbo wa Frank Ntulo (2017)

Mtunzi wa wimbo anawataka wanandugu wamhudumie mtu akiwa mgonjwa, wasisubiri afe ndio wagharimie maziko ya gharama kubwa. Mwimbaji anaeleza kuwa inawezekana kilichomuua marehemu si ugonjwa, pengine ni njaa. Mwimbaji anaiomba jamii kubadilika. Ianze kuwasaidia watu wakiwa wagonjwa na siyo kuchangisha mchango wakishafariki. Wimbo huu una funzo kubwa katika jamii yetu ya sasa nchini Tanzania, siyo kwa Wakinga tu.

Halikadhalika, elimu ya UKIMWI imekuwa ikielezwa kupitia mbolezi za Wakinga wakati wa msiba. Taarifa ya maambukizi ya UKIMWI ya mwaka 2007-2008 inaeleza kuwa Makete ilikuwa inaongoza nchini Tanzania kwa 16% ikifuatiwa na Dar es Salaam iliyokuwa na 9% (TACAIDS, 2017) na 11.4% mwaka 2016-2017 (Tanzania HIV Impact Survey, 2016-2017). Watu wengi wamefariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI na watoto wengi wameachwa yatima. Ufuatao ni wimbo

[4] Baadhi herufi katika lugha ya Kikinga zinaonekana zina kimsatari, kama zimekatwa. Huo ndio uandishi sahihi wa lugha ya Kikinga kwa herufi hizo. Utamshi wa herufi hizo hutofautiana na herufi iliyoandikwa kawaida. Uandishi na matamshi hayo haugusi herufi zote bali ni herufi chache ambazo ni 'i' na 'u'.

unaoelezea hali ilivyo katika jamii baada ya kukumbwa na UKIMWI:

| (7) *Gɨtamile Mibɨkɨ Gyene* | Imebaki Miti Mitupu |
|---|---|
| Kikinga | Kiswahili |
| 1. *K[5]: Kɨvɨlɨla Kɨvɨlɨla gɨtamile mibɨkɨ gyene* | 1. K: Kibilila kibilila imebaki miti mitupu |
| 2. *W: Kɨvɨlɨla Kɨvɨlɨla gɨtamile mibɨkɨ gyene x2* | 2. W: Kibilila kibilila imebaki miti mitupu x2 |
| Kiitikio | Kiitikio |
| 3. *Uwe kwawe tʉswe tʉsilile,* | 3. Sisi kwetu tumekufa tumeisha, |
| 4. *Uwe kwawe tʉswe tʉsilile mibɨkɨ gyene x2* | 4. Sisi kwetu tumekufa tumeisha miti mitupu x2 |

**Chanzo:** Data ya Uwandani, kijiji cha Maliwa (2017)

Maneno katika wimbo huo yanadokeza kuwa jamii ya Wakinga ni wapandaji wa miti ya mbao laini (mipaina) kwa ajili ya biashara. Wakinga wengi walifariki kwa ugonjwa wa UKIMWI, kwani watu walioipanda miti hiyo wamekufa imebaki miti mitupu.

### 4.2.6 Kuelezea Matatizo ya Jamii na Utatuzi wake

Jamii ya Wakinga imekuwa ikikabiliwa na changamoto kadha wa kadha. Miongoni mwa changamoto hizo ni hali duni za kiuchumi zinazotokana na miundombinu isiyo rafiki inayowanyima fursa ya kufikisha mazao sokoni kwa wakati. Aidha changamoto zingine ni baridi kali ambayo huathiri wanajamii na hasa watoto ambao hushindwa kuhudhuria masomo yao vizuri. Mbali na changamoto tajwa jamii ya Wakinga imepitia hali ya huzuni kwa muda mrefu kutokana na UKIMWI. Ugonjwa huu umesababisha wazazi na ndugu kufariki na kuacha watoto yatima na kupoteza nguvukazi ya taifa na familia. Kutokana na tatizo hili kuathiri jamii kwa kiasi kikubwa na kukosa tiba za kisayansi, baadhi ya wanajamii waliona kuwa suluhisho ni kwenda kwa waganga wa kienyeji. Wanajamii wengine waliona kuwa suluhisho ni kumwamini Mungu kama wimbo ufuatao unavyofafanua:

| (8) *Nding'ung'uta* | Nasikitika |
|---|---|
| Kikinga na Kiswahili | Kiswahili |
| 1. *Nyie vaputi mwiputage ndisoma mwe,* | 1. Enyi wachungaji muombe, nawasihi mwe, |
| 2. *ʉvʉpina wubangada ndilela mwe x2* | 2. Ukiwa unatesa nalia mwe x2 |
| 3. *Ʉmanga gumalile avanu ndilela mwe,* | 3. Ardhi imemaliza watu nalia mwe, |
| 4. *Amatsumba lwambʉlɨlo ndisagaa mwe,* | |

[5] K inamaanisha Kiongozi na W inamaanisha Wote.

5. *Avahotsi valongwe vadada mwe,*
6. *Nding'ung'uta ʉvʉpina ndilɨla mwe,*
7. *Nding'ung'uta mwe nding'ung'uta mwe,*
8. *Nding'ung'uta nding'ung'uta mwe, wivava ʉvʉpina*
9. *Yesu ni baba wa yatima ni mume wa wajane,*
10. *Musilie jipeni moyo nyieee,*
11. *Yatima nyie wajane musilie, Yesu yupooo,*
12. *Makanisa mko wapi yatimaa,*
13. *Mbona kila siku wao ni vilio…*

4. Siku zinapita nawaza mwe,
5. Wazazi wametangulia wazazi mwe,
6. Nasikitika ukiwa nalia mwe
7. Nasikitika mwe ukiwa nalia mwe,
8. Nasikitika nasikitika ukiwa unauma
9. Eeeh Yesu ni baba wa yatima ni mume wa wajane,
10. Musilie jipeni moyo nyie,
11. Yatimaa, ni wajeni, musilie, Yesu yupoo,
12. Makanisa mpo wapi yatimaaa,
13. Mbona kila siku wao ni vilio…

**Chanzo:** Data ya Maktabani, Wimbo wa Aldo Sanga (2017)

Wimbo wa *Nding'ung'uta* (*Nasikitika*) unaeleza kuwa ukiwa unauma. Wimbo huu uliimbwa msibani kupitia sabufa (zimerekodiwa na kuwekwa katika kinyonyi). Ujumbe uliomo katika wimbo huu ni kuwakumbusha wanajamii hali ya huzuni wanayopata wafiwa na hasa watoto wanapofiwa na wazazi wao. Mtunzi wa wimbo huu anaeleza kuwa wachungaji kupitia dini ya Kikristo wawasaidie wanajamii kuomba ili tatizo la uyatima liishe.

Mtunzi mwingine kupitia wimbo unaoitwa *Amalile Van'u Usetano* (Shetani Amemaliza Watu) anaeleza kuwa shetani ni mbaya, anamaliza watu wakiwa katika hatua mbalimbali (tumboni, wanaponyonya kwa mama zao na hata wakiwa wakubwa). Shetani ni dhana dhahania inayotumiwa na wanajamii kurejelea imani inayoamini kuwa mambo mabaya yanayowakumba wanajamii yanatokana na shetani. Maana hii inahusisha matendo ya ibada ya waabudu shetani ambao huombea mabaya yawapate watu wengine (Cambridge Dictionary, 2020). Shetani analaumiwa kwa kuwashawishi watu kufanya ngono zembe na hivyo watu huambukizwa UKIMWI. Hivyo husababisha watu kufa mapema, kuacha watoto yatima, kupoteza kipato na kupoteza nguvu kazi ya taifa. Kwa hiyo, watunzi wanaomba watu wa kada mbalimbali na wachungaji waombe sana ili watu wasipatwe na mabaya, hasa kifo. Aidha, dhima hii ya kuelezea matatizo na suluhisho yanayoikabili jamii inajidhihirisha zaidi kupitia wimbo wa *Amalile Van'u Usetano* (Shetani Amemaliza Watu) ulioimbwa na Aldo Sanga. Katika wimbo huu anasema shetani amemaliza watu kwa kuwaingiza katika vishawishi na kujiingiza katika mapenzi ya zaidi ya mwenza mmoja, hivyo wanaharibikiwa maisha na kukumbwa na mauti yanayotokana na UKIMWI. Mitazamo ya wanajamii inaonesha

kumlaumu shetani huku tafiti zinaonesha kuwa UKIMWI unatokana na ngono zembe, ambapo mtu huamua kuwa na mahusiano zaidi ya mwenza mmoja bila kinga kwa utashi wake binafsi (TACAIDS, 2008). Aidha, wahojiwa walieleza maambukizi makubwa ya UKIMWI hutokana na wanaume wengi wa jamii ya Kikinga kuwa wafanyabiashara na safari zao za mara kwa mara husababisha kuwa na mahusiano zaidi ya mpenzi mmoja. Wanaporudi kwa wake zao huwa wameambukizwa, na wao huwaambukiza wake zao, hatimaye watoto wanabaki yatima. Dhima ya mbolezi-nyimbo ni kuwaelimisha wanajamii kuwa wawe na mwenza mmoja mwaminifu ili kuepuka wa UKIMWI.

**4.2.7 Kujipatia Kipato kwa Watendaji wa Mbolezi**

Mbolezi katika jamii ya Wakinga zinatendwa kwa lengo la kujipatia kipato pia. Mbali na kuliwaza lakini watendaji hutegemea wapate kinywaji, chakula na pesa kupitia mbolezi. Katika kijiji cha Maliwa, watendaji wa mbolezi-nyimbo, maarufu kama *njʉlʉlʉ*, wanasema wazi kuwa wanatenda mbolezi ili kujipatia kipato. Hualikwa kutenda mbolezi na hulipwa malipo japo kidogo, ama sivyo huhudhuria msibani kama wanakijiji wengine tu. Mtoa taarifa mmojawapo anaeleza kuwa:

> Wananipa chochote kwamba uje tushereheke hii burudani hii (kujenga makaburi). Ni hela ndogo kama elfu hamsini, elfu ishirini, ishirini na tano. Wanasema tutakusafirisha sisi wenyewe. Kwa ndani ya kijiji wananilipa shilingi kumi na tano elfu, nje ya kijiji hulipwa elfu hamsini.

(Mahojiano Maliwa. tar. 25/08/2017)

Mtendaji anasema bila kulipwa chochote hatendi mbolezi kwa sababu utendaji wa mbolezi-nyimbo *njʉlʉlʉ* hutumia nguvu kubwa katika kucheza. Hivyo, malipo hayo yanawatia moyo na kuwapa ari ya kucheza zaidi. Pia, anasema ameshawahi kualikwa kutenda mbolezi kwa malipo maeneo ya nje ya Makete katika shughuli ya kujengea kaburi. Kwa sasa, suala la utendaji wa mbolezi kwa malipo si geni tena katika jamii. Imeshudiwa katika baadhi ya miji na majiji nchini Tanzania kumeundwa baadhi ya vikundi kwa ajili ya kuomboleza tu. Mfano kikundi kinachopatikana Mwananyamala kwa Mama Zacharia jijini Dar es Salaam (Bona TV, 2019; Cloudsmedia, 2020). Vikundi hivyo vinakodishwa kwa ajili ya kuomboleza msibani kwa malipo maalumu. Hivyo inawezekana katika jamii ya Wakinga hali ya kutenda kwa kutegemea kulipwa inaweza kukua zaidi kwa kuwa jamii huingiliana na huambukizana maarifa na sanaa.

Aidha, watendaji wengi wa mbolezi za Kikinga hawategemei sana kulipwa pesa, hiyo ni hiari ya mfiwa. Hata hivyo, desturi iliyopo ni kuwapa chai, pombe, soda na chakula. Wanasema kuwa vitu hivi ni muhimu kwa sababu huwawezesha

kufanya vizuri ingawa hawavidai. Wafiwa hutoa vitu hivi kama sehemu ya shukrani kwa kuimba na kucheza wakati wa msiba, kumaliza msiba, kujenga makaburi na kuhamisha wafu. Hata hivyo, suala la kujipatia kipato linadhihirika kwa baadhi ya wasanii kuanza kurekodi nyimbo na kuziweka katika mfumo maalumu kama vile sidii, vinyonyi na *Youtube* ambavyo vinawawezesha kuuza na hivyo kujipatia kipato. Baadhi ya wasanii waliorekodi ni pamoja na Frank Ntulo, Aldo Sanga, Ndezi Boy na Nesta Sanga kwa kuwataja wachache.

## 5.0 Hitimisho

Makala hii inadhirihisha kuwa mbolezi zina dhima mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuliwaza wafiwa, kuendeleza imani ya kuwa kuna uhai baada ya kifo, kuendeleza umoja na ushirikiano, kuonya na kukosoa mwenendo wa jamii, kuelimisha jamii, kuelezea matatizo ya jamii na utatuzi wake na kujipatia kipato kwa watendaji wa mbolezi. Baadhi ya maonyo yaliyomo katika mbolezi za sasa yanahusu mambo mbalimbali katika jamii iliyopo sasa, kusisitiza ushirika wakati wa misiba, kuonya juu ya mitala, kupinga wachawi na kujihadhari na UKIMWI. Aidha, makala hii imeweka bayana kuwa ili kuelewa kwa undani dhima za mbolezi ni vema kutumia mbinu mbalimbali katika ukusanyaji wa data badala ya kuchambua mashairi ya mbolezi pekee. Pia, ipo haja ya kuandika makala nyingine zinazohusisha jamii mbalimbali za nchini Tanzania ikiwamo miji mikubwa ili kupata dhima mbalimbali za mbolezi kama zinavyoelezwa na watendaji wa mbolezi hizo.

## Marejeleo


Amanyisye, K.T. (2017). Kuchunguza Dhima ya Nyimbo kwa Wafiwa katika Jamii ya Wanyakyusa Wilaya ya Rungwe, Mkoa wa Mbeya. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Bona TV (2020). “Hichi Ndio Kikundi cha Kulia Misibani/Aina Nne za Vilio na Bei Zake Wazitaja.” Katika https://youtu.be/GwtVFsDsiZs. Imesomwa Julai 26, 2020.

Cambridge Dictionary (2020). *English Dictionary*. Cambridge University Press.

Cloudsmedia TV (2020). Kwa Wenye Misiba Hii Ndio Bei ya Vilio! Wachaga Wahaya Ndio Wateja Wakubwa, https://youtu.be/Z4tSrMwv1WM. Imesomwa Julai 26, 2020.

Finnegan, R. (2012). *Oral Literature in Africa*. PB - Open Book Publishers.

Finnegan, R. (2017). *Oral literature in Africa*. Open Book Publishers.

Hakola, O., and Kivistö, S. (2014). *Death in Literature*. Cambridge Scholars Publishing.

Kidane, W. (2012). Function of Funeral Dirges and Interpretation of Death in Kaficho Poetry.Thesis, Addis Ababa University.

Mbiti, J. (1969). *African Religion and Philosophy*. Nairobi: Heimann Educational BooksLimited.

Mbiti, J. (1991). *Introduction to African Religion*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

McCaskie, T.C. (1989). “Death and the Asantehene: a Historical Meditation.” *The Journal of African History*. *30*(3): 417-444.

Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: OUT.

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Ojaide, T. (2005). *A Creative Writing Handbook for African Writers and Students*. Lagos: Malthouse Press.

Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature: Backgrounds, Character and Continuity*. Bloomington: Indiana University Press.

Pagalo, G. (1996). Imani ya Wakinga Juu ya Lwembe na Uhusiano wake na Ukristo katika Dayosisi ya Kusini Kati. Kozi ya Cheti (Haijachapishwa). Chuo cha Kilutheri cha Theolojia Makumira.

Platt, L.A., & Persico, V.R. (1992). *Grief in Cross-cultural Perspective: A Casebook*. New York: Garland Pub.

TACAIDS (2008). Tanzania HIV/AIDS and Malaria Indicator Survey 2007-08. Dar es Salaam: TACAIDS, ZAC, NBS, OCGS, and Macro International Inc.

TACAIDS (2017). National HIV and AIDS Response Report for 2017 Tanzania Mainland.Dar es Salaam: Tanzania Commission for AIDS

Tanzania HIV Impact Survey, (2016-17): https://phia.icap.columbia.edu/wp-content/uploads/2017/11/Tanzania_SummarySheet_A4.English.v19.pdf . Imesomwa Juni 10, 2020.

Tempels, P. (1959). *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.

Urquiza, E. and Kotrschal, K. (2015). “The Mind Behind Anthropomorphic Thinking: Attribution of Mental States to Other Species.” *Animal Behaviour*. 109: 167-176.